

SHULE YA UPILI YA KIPSUTER

MTIHANI I MUHULA II, 2017

KIDATO CHA PILI

KISWAHILI

Jina: _____ Nambari: _____ Darasa: _____ Tarehe: _____

Maagizo:

i). Hakikisha kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa

sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

ii). Jibu Maswali yote kwenye nafasi ulizoachiwa.

1. Taja sauti mbili mbili zenye sifa zifuatazo:

a) Sauti za ufizi. (alama 1)

b) Sauti za meno. (alama 1)

2. Tunga sentensi moja moja ukitumia nomino zifuatazo:

a) Za dhahania. (alama 1)

b) Za kitenzi-jina. (alama 1)

3. Bainisha aina za maneno katika sentensi hii.

Salaale! Nyoka hatari mno amepanda juu ya mti. (alama 4)

4. Yakinisha sentensi ifuatayo:

Chakula hakipikiki vizuri. (alama 1)

5. Kanusha:

Ningalikuwa na uwezo ningalinunua pikipiki. (alama 1)

6. Andika katika hali ya wingi:

Kuku yuyu huyu ndiye aliyetaga yai hili. (alama 2)

7. Weka nomino zifuatazo katika ngeli zao: (alama 3)

a) Daraja

b) Uovu

c) Mate

8. Tenga viambishi katika neno lifuatalo na utaje majukumu vinavyotekeleza.

Niliyempelekea. (alama 3)

9. Akifisha tungo ifuatayo:

je utaenda kitale siku alhamisi patel aliuliza(alama 4)

10. Andika ukubwa na udogo wa (alama 2)

	Ukubwa	Udogo
Nyumba		

11. Tambua na utaje aina ya vivumishi katika sentensi ifuatayo:

Chakula kingi kilipakuliwa wageni wale. (alama 2)

12. Onyesha silabi inayotiliwa mkazo katika neno hili:

Utelezi. (alama 1)

13. Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya mistari au mishale.

Mkulima hodari alipalilia mahindi yake sana. (alama 3)

*****HUU NI UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA*****